

MKATABA WA UPANGAJI  
**MKATABA HUU umefanyika leo tarehe 31 Mwezi AGOSTI, 2024.**  
**KATI YA**

**Simon Baron Mwhanga wa S.L.P 8715 Dar es Salaam** (hapo baadaye kurejewa kama *MWENYENUMBA*) kwa upande mmoja.

NA

**Soric Investment Limited wa S.L.P 80383 Dar es Salaam** (hapo baadaye kurejewa kama *MPANGAJI*) kwa upande mwingine.

*KWA KUWA* mwenyenyumba ni mmiliki halali wa nyumba iliyoko mtaa wa Muhonda kiwanja Na.37,Kitalu "E" Ilala-Dar es Salaam (hapo baadaye kurejewa kama 'Nyumba').Na anapangisha chumba husika kama kilivyo.

*NA KWA KUWA* Mpangaji yuko tayari na anahitaji kupanga chumba kwenye nyumba tajwa iliyopo katika eneo husika kwa masharti ya mkataba huu.

**BASI MKATABA HUU UNASHUHUDIA YAFUATAYO:-**

1. *KWA KUZINGATIA MALIPO* ya kodi ya pesa za Kitanzania Shilingi laki mbili tu,(TSHS. 300,000/=) kwa mwezi, basi mwenye nyumba anampangisha mpangaji kwa kipindi cha muda wa miezi sita kuanzia tarehe 31/08/ 2024 mpaka tarehe 28/02/ 2025.
2. *Kwamba siku ya kutia saini mkataba huu mpangaji amelipa kodi yote ya miezi mitatu shilingi laki sita tu. (TSHS. 1,200,000/=) na mwenyenyumba anakiri kupokea pesa hizo.*
3. Mpangaji atatakiwa atoe taarifa ya miezi mitatu kabla ya mkataba kuisha kama ataendelea na upangaji wake.
4. Kwamba mpangaji haruhusiwi kumpangisha mtu mwingine bila ya taarifa kwa mwenye nyumba.
5. Gharama ya umeme,maji,ulinzi na usafi zitamhusu mpangaji.
6. Kwamba mpangaji atamjulisha mwenye nyumba kwa kumpa NOTISI ya maandishi ya siku tisini(90),kabla ya mkataba kumalizika,ikiwa atataka kusitisha mkataba huu.
7. Kwamba iwapo tatizo lolote litajitokeza basi sharia za nchi zitatumika kutatua mgogoro huu.

Makubaliano haya yametiwa sahihi hapa Dar es Salaam na pande zote zinazohusika leo hii tarehe 31, Agosti, 2024

MKATABA umesainiwa na .....  
ambaye ninamfahamu

binafsi, leo hii tarehe 31/08/2024

*Simon Baron*

MWENYE NYUMBA

SAHIHI



**ANUANI S.L.P 3373 DSM**

DAR ES SALAAM  
SIFA WAKILI



MKATABA umesainiwa **na**.....

ambaye ninamfahamu binafsi,  
leo hii tarehe 31/08/ 2024

*MPANGAJI*

MPANGAJI

SAHIHI



**ANUANI S.L.P 3373 DSM**

DAR ES SALAAM  
SIFA WAKILI



